2. **Mhandisi wa Vifaa Tiba daraja la II (Biomedical Engineer grade II)**
NAFASI (1)

a) **SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe na cheti cha kidato cha nne au kidato cha sita, stashahada au shahada ya Sayansi ya uhandisi wa vifaa Tiba (Biomedical Engineering) kutoka chuo kinachotambulika na NACTE
- Awe na ujuzi wa kutumia na kutengeneza vifaa vya kitabibu vya kielektroniki na vya umeme.
- Awe na uelewa wa msingi wa kompyuta na program zinazotumika katika ufuatiliaji wa vifaa vya tiba.
- Uwezo wa kufanya kazi katika mazingira yoyote.
- Awe tayari kufanya kazi kwa muda wa ziada au kufika kazini haraka endapo kutatokea dharura ya kifaa muhimu kuharibika.

b) **MAJUKUMU YA KAZI**

- Kufanya matengenezo ya mara kwa mara na ukarabati wa vifaa vya tiba vya hospitali ili viwe katika hali nzuri ya kufanya kazi muda wote.
- Kuimika (install) na kujaribu (test) vifaa vipya vya tiba vinavyowasili hospitalini kan=bla ya kuanza kutumika.
- Kutunza kumbukumbu za vifaa vya tiba, ikiwemo tarehe za matengenezo na hali ya kifaa.
- Kushirikiana na wauguzi na madaktari kuhakikisha vifaa vinatumiwa ipasavyo na kwa usalama.

Archdiocese of Arusha
wasso hospital

- Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu ununuzi, matumizi, na uboreshaji wa vifaa vya tiba vipya.
- Kuhakikisha kanuni na miongozo ya usalama wa vifaa vya umeme na vya kitabibu inazingatiwa.
- Kutayarisha ripoti za matengenezo, ukaguzi wa vifaa, na mapendekezo ya bajeti ya vifaa vya kitabibu.
- Kufanya mafunzo mafupi (orientation) kwa watumishi wanaotumia vifaa vya tiba vipya.

**MASHARITI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45.
ii. Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI.
iii. Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa .Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au kitambulisho cha mpiga kura.
iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
v. **Testimonials, Provisional Results, Statement of Results, hati ya matokeo ya kidado cha nne na sita (FORM IV AND VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
vi. **Waombaji waliosoma nje ya Tanzania Wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).**
vii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
viii. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 30 Novemba, 2025.**
ix. **Maombi yawasilishwe kwa njia ya barua kwa Mganga Mfawidhi Hospitali ya Wasso S. L.P. 42, LOLIONDO, barua pepe. secretary@wassohospital.org**

MEDICAL OFFICER INCHARGE WASSO DDH. P. O. Box 42 LOLIONDO ARUSHA

.....................................

Dkf Kasorima Elikana

**MGANGA MFAWIDHI**